

**BIASHARA**

**Serikali imejitolea kufufua shirika lake la kupitisha mizigo lililokwama**

Uk 3




**TEKNOLOGIA**

Mpango wa KFCB kuwezesha walezi na ujuzi wa kutunza watoto

UK 4

**UHAMASISHAJI**

**Watetezi wa haki za watoto wapata hali ngumu kurejesha waathiriwa wa dhuluma za kijinsia katika hali yao ya kawaida**



Uk 6

www.mygov.go.ke

FEBRUARI 14, 2023

MyGov.

TATHMINI YAKO YA WIKI

Issue No. 31/2022-2023

# Watafiti KALRO waunda bidhaa kupunguza kuvu katika chakula

Mkurugenzi Mkuu wa KALRO Dkt. Eliud Kireger asema watafiti wameunda bidhaa inayoitwa 'Aflasafe KE01' ya kibaiyolojia na ambayo inaondoa fangasi katika mchanga

**NA WANGARI NDIRANGU (KNA)**

Shirika la Utafiti wa Kilimo na Ufugaji Kenya (KALRO) na wadau wengine wametengeneza bidhaa ya kibaiyolojia inayoitwa 'Aflasafe KE01,' ambayo inamaliza fangasi inayotoa kuvu katika mchanga.



Kuvu ni sumu inayotolewa na fangasi inayoishi katika mchanga na huambukiza mimea ikiwa shambani na hivyo basi kuathiri sekta ya kilimo kote nchini, huku mahindi na njugu ziliathiriwa zaidi. Akizungumza katika warsha ya kufahamisha aflasafe Mkurugenzi Mkuu wa KALRO Dkt Eliud Kireger alisema kwamba, hatua hiyo inajiri baada ya wakulima, wafanyabiashara na mashirika mengine kupata hasara kubwa kutokana na fangasi inayoharibu nafaka na kuifanya usiweze kufaa kwa matumizi ya binadamu. Hii inasababisha athari pana ikiwemo kupungua kwa

ENDELEA UK 2




**Shirika dogo la Roam, awali likijulikana kama Opibus limeanzisha basi jipya la kutumia umeme, Roam Rapid, ambalo limeundwa kushughulikia changamoto za kipekee katika uchukuzi wa umma Nairobi na kwingineko barani Afrika. Picha|HISANI**

**Takwimu za Wiki**

**30,000**
Idadi ya familia zitakazonufaka na mradi wa bima ya mifugo katika kaunti ya Kajiado

**500M**
Makadirio ya mapato Government Clearing Agency (GCA) inatarajiwa kupata kwa mwaka

**4.2M**
Idadi ya mifugo ambao wameangamia miongoni mwa jamii za wafugaji kufuatia ukame

**100**
Tani za vidonge ambavyo kampuni ya Powerspot Pelletizers imetengeneza kutokana na masalia ya miwa Kakamega

**29**
Aina mpya ya mihogo ambayo inahimili magonjwa na kiangazi ambayo Egerton University imetengeneza

# Serikali yatafiti uhusiano wa dawa za kuua wadudu na visa vya saratani

**NA SAMUEL MAINA NA YVETTE NJERI(KNA)**

Utafiti unaendelea kubaini uwekezekano wa uhusiano wa matumizi ya dawa za kuua wadudu kwenye mimea na kuongezeka kwa visa vya saratani hasa katika eneo la Mlima Kenya.

Mwenyekiti wa Shirika la Ukaguzi wa Afya ya Mimea( KEPHIS) Bw Peter Weru anasema kwamba, utafiti huo, ambao utafanywa katika kaunti 10 za Kati ya Kenya utasaidia Serikali kuanzisha hatua za kuzuia pembejeo hatari za shambani katika eneo hilo.

Ripoti ya Wizara ya Afya ya mwaka 2022 ilifichua kwamba kaunti za Nyeri,



Peter Weru

Murang'a, Kirinyaga na Embu, zina mzigo mkubwa wa saratani nchini.

Wakati huo huo, visa vya saratani kaunti ya Nyeri vilikuwa 2,127 kwa kila watu 100,000 huku Murang'a ikiwa na visa 2,123 ikifuatwa na Kirinyaga ikiwa na visa 2,033.

Zingine ni (1,783), Meru (1,789), Nyandarua (1,776), Tharaka Nithi (1,644) na Nakuru (1,612).

"Tunashirikiana na kaunti zote kumi zinazounda Jumuiya ya Uchumi ya Mlima Kenya kutegua kitendawili cha ongezeko la idadi ya visa vya saratani katika eneo hili na iwapo ongezeko hilo linahusiana kwa njia yoyote na matumizi ya kemikali kwa mimea ya chakula," Weru aliambia wanahabari alipomtembelea Gavana Mutahi Kahiga katika ofisi yake.

Weru pia alishukuru kaunti ya Nyeri kwa kutoa

ENDELEA UK 2

KOMESHA COVID-19
“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”
HOMA
KIKOHOZI
KUSHINDWA KUPUMUA
MAUMIVU KOONI
KUUMWA NA KICHWA

# Watafiti KALRO waunda bidhaa kupunguza kuvu katika chakula

ENDELEA KUTOKA UK 1

uzalishaji wa wanyama, gharama ya juu ya kuondoa sumu hiyo na kuharibiwa kwa mazao yaliyo na sumu.

“Bidhaa imeonyesha uwezo mkubwa wa hadi asilimia 98 wa kupunguza kuvu katika mahindi na ina uwezo wa kudumisha viwango vya chini vya sumu hiyo, kabla na baada ya kuvuna,” alieleza.

“Kuvu pia hutumika kama kizingiti kisicho cha ushuru kwa biashara ya humu nchini, kikanda na kimataifa kwa kuwa eneo ambalo mazao yanashukiwa kuwa nayo yanagunduliwa mara moja huwa linapoteza soko au linawekwa chini ya ukaguzi mkali,” alisema.

Dkt Kireger alisema kuna haja ya kushinikiza kukubaliwa kwa bidhaa za Aflasafe kupitia kandarasi na Koppert Biological Limited chini ya ushirikiano wa sekta ya umma na kibinafs (PPP) ili isambaze bidhaa hiyo ambayo matumizi yake yangali ya chini.

Alisema warsha hiyo ya kufahamisha ilinuiwa kuelewa ripoti na utathmini wa



Mkurugenzi Mkuu wa KALRO, Dkt Eliud Kireger (kushoto) Nina Javanovic na Prof Jake Ricker wazungumzia jambo.

uwezo, mahitaji na kuinua uwezo wa Aflasafe katika Kenya, hasa kaunti za Meru na Tharaka Nithi ambazo ni baadhi ya maeneo yaliyoathiriwa vibaya.

Alihimiza wadau, hasa katika mifumo ya thamani ya mahindi kuhakikisha wanazungumza na wakulima zaidi kuhusu matumizi ya aflasafe ambayo yanaathiri afya za watu yakipata simu hiyo.

> Mahindi yaliyoharibika kawaida hupewa mifugo hali ambayo ni hatari” -Kireger

“ Mahindi yanayoathiriwa kwa kawaida huwa yanapatiwa mifugo lakini athari zinapitishwa kwa binadamu kupitia matumizi ya bidhaa kama maziwa, mayai na nyama. Umuhimu wa kiuchumi wa kuvu hasa kwa mahindi hivyo basi, hauwezi kusisitizwa zaidi,” akasema Dkt Kireger.

Aliongeza kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi na kupanda kwa joto, visa vya kuvu ambavyo vilikuwa katika maeneo kame ya Meru ambako viwango vya joto ni zaidi ya nyuzi 25, sasa vinapatikana Trans Nzoia na hata Bungoma ambazo hazikujulikana kuwa na kuvu.

# Serikali yatafuta uhusiano wa dawa za kuua wadudu na visa vya saratani

ENDELEA KUTOKA UK 1

kipande cha ardhi kwa ujenzi wa ofisi ya kikanda ya KEPHIS, kutumiwa na wafanyakazi wake na kuwezesha juhudi za kuhakikisha wakut wanapata mbegu salama na bora.

Alisema kwamba hatua hiyo itaongeza uzalishaji wa chakula katika eneo hilo na pia kuhakikisha mimea ya biashara kutokana eneo hilo imetimiza viwango vya usalama vya kimataifa.

Oktoba mwaka jana, Shirika lisilo la kutengeneza faida la Ujerumani (NGO), lilihimiza kukomeshwa kwa uagizaji wa kemikali za kuua wadudu ambazo zimetajwa kuwa sumu. Heinrich-Böll-Stiftung lilidai kwamba takwimu zilionyesha kwamba asilimia 76 ya kemikali za kuua wadudu zinazotumiwa Kenya ziko na kiungo kimoja au zaidi kinachoorodheshwa kama Kemikali Hatari Zaidi (HHPs). Shirika hilo lilisema kemikali kama hizo ( kwa wakati huu



zimepigwa marufuku katika nchi za Ulaya) zimehusishwa na ongezeko la visa vya saratani, kuvuruga mifumo ya homoni na Neva na kuathiri jeni watoto kabla ya kuzaliwa.

Akizungumza katika hafla ya kuzindua Pesticide Plus, jarida kuhusu kemikali hatari, Mkurugenzi wa Heinrich-Böll-Stiftung Joachim Paul alisema kemikali ambazo zimepigwa marufuku Ulaya bado zinauzwa Afrika.

“Kemikali ambazo haziruhusiwi kutumiwa katika nchi kama Ujerumani zinakotengenezewa bado zinauzwa katika nchi zingine za nje. Nchini Kenya, asilimia 44 ya kemikali zote zinazotumiwa zimepigwa marufuku Ulaya,” alisema kwenye taarifa kwa vyombo vya habari.

REPUBLIC OF KENYA
RBA Retirement Benefits Authority

TAARIFA KWA WADAU WA MPANGO WA MAFAO YA KUSTAAFU

MKATABA-KUTOKA KWA WAAJIRI CHINI YA SHERIA YA HAZINA YA MALIPO YA UZEENI 2013

Kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 21 na Jedwali la Nne la Sheria ya Hazina ya Malipo ya Uzeeni Namba 45 ya mwaka 2013 iliyoanza kutumika tarehe 1 Juni 2014, na uamuzi wa Mahakama ya Rufaa uliotolewa tarehe 3 Februari 2023, Mamlaka ya Mafao ya Kustaafu ingependa kuwafahamisha Waajiri, Wadhamini na Wasimamizi wa Miradi ya Mafao ya Kustaafu yafuatayo:

1. Kanuni za Hazina ya Malipo ya Uzeeni (Mkataba kutoka kwa Waajiri) 2014 sasa zimeanza kutumika.
2. Waajiri wanaotaka kutuma michango ya Daraja la II katika mpango wa mkataba kama ilivyoainishwa chini ya Kifungu cha 21 cha Sheria ya NSSF wanaweza kutuma maombi kwa Mamlaka ya Mafao ya Kustaafu.
3. Waajiri watahitajika kuwasilisha Fomu C1 iliyojazwa ipasavyo pamoja na viambatisho vinavyohitajika vilivyorejelewa kwenye fomu ili kuzingatiwa na Mamlaka ya Mafao ya Kustaafu.
4. Ili mpango ufuzu kupokea michango ya Daraja la II kama ***“mpango wa nje ya mkataba”*** wanatakiwa kutimiza Jaribio la Mpango wa Marejeleo. Mamlaka itatoa Cheti cha Mpango wa Marejeleo kwa Skimu ambazo zimekidhi sifa zilizotajwa.
5. Fomu ya maombi, Fomu C1 na Kanuni za Hazina ya Kitaifa ya Malipo ya Uzeeni (Mkataba Kutoka kwa Waajiri) 2014 zinaweza kupakuliwa kutoka kwenye tovuti ya Mamlaka, ***www.rba.go.ke.*** Fomu ya maombi pia inaweza kuchukuliwa kutoka kwa afisi zetu.

**MAMLAKA YA MAFAO YA KUSTAAFU**
**Rahimtulla Tower, Oorofa ya 13, Upper Hill Road, P.O. Box 57733-00200 Nairobi**
**Simu: 2809000; Simu ya rununu 0726 600001-5 au 0735 339132**
**Barua pepe: info@rba.go.ke; Tovuti: www.rba.go.ke**

**For more, follow us on:-**

twitter: @RBA_Kenya
Instagram: rbakenya
facebook: @RetirementBenefitsAuthorityKE
linkedin: Retirement Benefits Authority Kenya
YouTube: Retirement Benefits Authority
Email: info@rba.go.ke
Website: www.rba.go.ke

***Retirement Benefits Authority (RBA) is ISO 9001: 2015 Certified***

REPUBLIC OF KENYA
NTSA Keep our roads safe
National Transport and Safety Authority

MWALIKO WA ZABUNI

Mamlaka ya Kitaifa ya Usafiri Salama inakaribisha wazabuni wanaostahiki kwa zabuni zilizoorodheshwa hapa chini:

| S/ No | Namba ya Zabuni: | Maelezo ya Zabuni | Uhitimu | Kufunga | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Tarehe | Wakati |
| 1. | NTSA/NCB-013/2022-2023 | Utoaji wa Huduma za Usafishaji, Ukusanyaji taka na Ufukizaji kwa Makao Makuu ya Mamlaka ya Kitaifa ya Usafiri Salama na Ofisi za Mikoa (Mkataba wa Mfumo wa Miaka Miwili). | Imetengewa Vijana, Wanawake na Walemavu | Februari 14, 2023. | saa 11.00 asubuhi |

Waombaji wenye nia wanaweza kupata maelezo zaidi kutoka na kukagua hati za zabuni katika **Afisi ya Ununuzi, Makao Makuu ya Mamlaka ya Kitaifa ya Usafiri Salama Barabarani , orofa ya 8, 316 Upper Hill Chambers 2nd Ngong Avenue** wakati wa saa rasmi za kazi- (8.00 asubuhi - 1.00 mchana, 2.00 mchana - 5.00 jioni).

Seti kamili ya hati za zabuni kwa Kiingereza zinaweza kupakuliwa kutoka kwa tovuti yetu kwa **http://www.ntsa.go.ke** au **http://www.tenders.go.ke** ***bila malipo***. Wazabuni wanaopakua hati zabuni lazima wapeleke maelezo yao mara moja kwa procurement@ntsa.go.ke kwa rekodi na mawasiliano ya **ufafanuzi/ziada zozote za zabuni.**
Hati zilizokamilishwa za zabuni zinapaswa kuambatanishwa katika bahasha wazi, zilizofungwa na zilizo na nambari ya kumbukumbu ya zabuni na kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni kwenye **orofa ya 8, 316 Upper Hill Chambers 2nd Ngong Avenue Nairobi au kutumwa kwa Mkurugenzi Mkuu, P.O Box 3602-00506 Nairobi** ili kupokelewa kabla au kabla ya tarehe na wakati ulioonyeshwa kwenye jedwali hapo juu.

Bei zilizotajwa zinapaswa kujumlisha ushuru na gharama zote za uwasilishaji na lazima ziwe katika Shilingi za Kenya na zitasalia halali kwa siku 126 kuanzia tarehe ya kufungwa kwa zabuni. Wazabuni lazima wahakikishe kuwa kila zabuni inayowasilishwa inasasishwa kutoka ukurasa wa kwanza hadi wa mwisho ikijumuisha viambatisho vyovyote.

Zabuni zitafunguliwa mara baada ya hapo mbele ya Wagombea au wawakilishi wao wanaochagua kuhudhuria katika Chumba cha bodi kilicho kwenye **orofa ya 9, 316 Upper Hill Chambers.**
Wazabuni wanaovutiwa wanatakiwa kuendelea kuangalia Tovuti ya Mamlaka ya Kitaifa ya Usafiri na Usalama **http://www.ntsa.go.ke** kwa maelezo/ufafanuzi wowote wa ziada ambao unaweza kutokea kabla ya tarehe ya kuwasilisha.

Ombi la yeyote atakayepatikana akidanganya litafutiliwa mbali.

**MKURUGENZI MKUU**

***www.ntsa.go.ke***

# Serikali imejitolea kufufua shirika lake la kupitisha mizigo lililokwama

NA HUSSEIN ABDULLAHI NA ANDREW HINGA (KNA)



**Katibu wa Shughuli za Meli na Maswala ya Baharini, Shadrack Mwadime (kulia) ahutubia wafanyakazi wa Government Clearing Agency mjini Mombasa. Katibu alisema shirika hilo la kiserikali litafufuliwa tena.** PICHA: ANDREW HINGA (KNA)

Serikali imejitolea kubadilisha Shirika la Kushughulikia Mizigo la Serikali (GCA) lililokufa kuwa taasisi ya kuleta mapato ndani ya miaka mwili ijayo.

Katibu wa Wizara ya Masuala ya Ubaharia Shadrack Mwadime, alisema kwamba shirika hilo linaweza kuleta mapato ya thamani ya Sh500 milioni kila mwaka kupitia utoaji wa huduma za kupitisha na kusafirisha mizigo.

"Tunataka kufufua GCA na kuirejesha katika hali yake ya mwanzo kwa kuzingatia ukweli wa hali ya sasa," alisema, na kuongeza kuwa litaundwa kuwa la viwango vya kisasa vya kkimataifa

Akizuru makao makuu ya shirika hilo katika eneo la Shimanzi, Mombasa, Mwandime alisema kwamba kufufua shughuli za shirika hilo kutaokoa pesa nyingi za serikali zinazotumiwa kama ada ambazo serikali inalipa mashirika ya kibinafsi ya kupitisha mizigo kwa mizigo inayoagiza kutoka nje ya nchi.

Bw Mwandime alisema kwamba hatua hiyo itafufua shirika hilo la kupitisha mizigo pia itahakikisha usalama na siri katika kupitisha mizigo muhimu ya serikali.

> Tunajitolea kufufua GCA na kurejesha hadhi yake ya zamani" - Mwadime

Katibu alisema kwamba kipaumbele cha serikali ni kufufua na kuimarisha taasisi ambazo ziko na uwezo wa kuchangia kwa uchumi wa nchi na kuinua maisha ya Wakenya GCA lilikuwa idara iliyonuiwa kupitisha mizigo ya serikali ya Wizara, Idara na Mashirika. (MDAs).

Kwa bahati mbaya, jukumu hilo halitekelezwi kikamilifu huku MDAs zikiamua kuhakikisha kwamba mizigo inapitishwa kupitia maajenti wa kibinafsi wa kupitisha mizigo kwa sababu ya utepetevu wa GCA.

Mwandime alifichua kwamba katika serikali ya sasa, majukumu ya GCA yamehamishiwa Wizara ya Fedha na kukabidhiwa Idara ya Shughuli za Ubaharia. Majukumu hayo yanahusu upitishaji na uchukuzi wa mizigo inayosafirishwa kupitia bahari, hewa na ardhi inayoagizwa na serikali.

# Familia 30,000 kunufaika na mpango wa bima ya mifugo

NA DIANA MENETO (KNA)

Serikali ya kaunti ya Kajiado kwa ushirikiano na Benki ya Dunia na Idara ya Serikali ya Mifugo imeanzisha Mpango wa Bima ya Mifugo kukinga wafugaji dhidi ya hasara zaidi huku hali ya ukame ikiendelea kuwa mbaya zaidi eneo hilo.

Akizungumza na wanahabari katika ofisi yake Kajiado, Gavana Joseph ole Lenku alisema familia 30,000 zitanufaika na mradi wa Bima ya Mifugo.

"Familia 20,000 zitawekewa bima ya mifugo yao bila malipo kwa hisani ya Benki ya Dunia huku familia zingine 10,000 zikilipa ada zilizopunguzwa mno ili mifugo yao iweze kuwa na bima," alisema Ole Lenku.

Kaunti hiyo imegawanywa katika maeneo manane kwa kulenga maeneo ya kuhamahama ambayo wakazi wanahusika na mfumo wa thamani wa nyama kuwezesha utekelezaji wa mradi huo.

Maeneo hayo manane ni; Iloodokilani linalojumuisha wadi za Magadi na Iloodokilani, Kaputiei linalohusisha wadi za Isinya, Kaputiei Kaskazini, Oloorsikon Sholinke na Kitengela. Kiek Onyokie linalojumuisha wadi za Kiek Onyokie, Mosiro na Ewuaso, Kuku linalojumuisha wadi za Kuku, Rombo na Kimana.

Maeneo mengine ni; Merrueshi linalojumuisha wadi za Poka Kenyawa na Imbirikani. Matapato likiwa na wadi za Matapato Kaskazini na Kusini, Olgulului linalohusisha wadi ya Entonet na Eselenkei na Olkeria linalojumuisha wadi za Ildamat, Ildalalekutuk na Imaroro.

"Mchakato huo unaanza Jumatatu na maafisa wa mifugo kutoka idara ya mifugo wataongoza shughuli hiyo wakisaidiwa na machifu na wasimamizi wa vijiji na panapowezekana ili wanaofaidi mpango huo wafanye hivyo kwa haki," aliongeza Gavana.


REPUBLIC OF KENYA

Kenya Power

## MWALIKO WA ZABUNI

Kenya Power inakaribisha zabuni kutoka kwa wazabuni wanaovutiwa kwa yafuatayo:-

| NO. | NAMBA YA ZABUNI | MAELEZO YA ZABUNI | TAREHE YA KUANZA ZABUNI | KIKAO / KUZURU ENEO | TAREHE YA KUFUNGA ZABUNI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | KP1/9A.2/OT/ 034/ICT/22-23 | Kupata na Kutekeleza Seva za Jina la Kikoa na Ngome za Mtandao wa ISP wa KPLC | Jumatano 15.02.2023 | N/A | Jumatano 08.03.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 2. | KP1/9A.2/OT/ 031/ICT/22-23 | Utoaji wa Matengenezo ya Minara ya Mawasiliano | Alhamisi 16.02.2023 | N/A | Alhamisi 09.03.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 3. | KP1/9A.3/OT/ 008/22-23 | Ufungaji, Usambazaji na Uwekaji wa Jenereta ya Ziada ya kVA 300 katika Kituo cha Umeme cha Kiunga | Alhamisi 16.02.2023 | N/A | Alhamisi 09.03.2023 saa 10.00 asubuhi |
| 4. | KP1/9A.2/OT/ 044/NM/22-23 | Ukarabati wa Usafirishaji na Usambazaji Miundo ya Chuma Iliyoharibika | Ijumaa 17.02.2023 | Alhamisi 23.02.2023 | Alhamisi 16.03.2023 saa 10.00 asubuhi |

Kwa Zabuni Na.4, kutakuwa na Mkutano wa Matayarisho ya Awali na Ziara za Lazima za Eneo katika:

1. Alhamisi 23.02.2023 katika Olkaria Generation Complex 32km kutoka Barabara ya Naivasha kwenye Barabara ya
Moi South Lake kuanzia saa 9.00 asubuhi hadi saa 2.00 alasiri
2. Jumatano 01.03.2023 huko Makupa - Mombasa kutoka saa 9.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni
3. Alhamisi 02.03.2023 huko Makande - Mombasa kuanzia saa 9.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni

Kwa Zabuni Na.5, kutakuwa na Mkutano wa Matayarisho ya Awali na Ziara za Lazima za Eneo katika:

1. Jumanne 28.02.2023 katika Kituo Kidogo cha Tononoka 33/11kV kutoka saa 9.00 asubuhi hadi saa 1.00 jioni
Nyaraka za zabuni zinazoelezea mahitaji ya zabuni zilizo hapo juu zinaweza kupatikana kutoka kwa tovuti ya Kenya Power (www.kplc.co.ke) kuanzia tarehe zilizoonyeshwa hapo juu.

**MENEJA MKUU**
**MFUMO WA USAMBAZAJI NA VIFAA**

**www.kplc.co.ke**

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy



REPUBLIC OF KENYA

KENYA POWER PENSION FUND

## TANGAZO LA ZABUNI

Hazina ya Pensheni ya Kenya Power inakaribisha mashirika kwa yafuatayo;

| NO. | JINA LA ZABUNI | NAMBA YA ZABUNI | UHITIMU | TAREHE YA KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | USHAURI WA MARUDIO YA MUUNDO WA SHIRIKA | KPPF/PROC/2-E/01/2023 | WAZI | Alhamisi Machi 2, 2023 saa 11.30 asubuhi |
| 2. | MKATABA WA MFUMO WA MIAKA MITATU WA UTOAJI WA MKUTANO NA HUDUMA ZA HOTELI. | KPPF/PROC/2-A/04/2023 | WAZI | Ijumaa Machi 10, 2023 11.30 asubuhi |

Hati za zabuni zinazoelezea mahitaji ya zabuni iliyo hapo juu zinaweza kupakuliwa kutoka tovuti ya Hazina **www.kppf.co.ke** kuanzia **Jumanne tarehe 14 Februari 2023** bila malipo yoyote. Wazabuni wanahitajika kujisajili kwa kutuma barua pepe kwa **tenders@kppf.co.ke** ili kupokea ufafanuzi na/au mawasiliano, inapohitajika.
Hati zilizokamilishwa za Zabuni katika bahasha zilizofungwa wazi zilizo na alama ya **jina la zabuni** na **nambari ya zabuni** zinapaswa kutumwa kama ifuatavyo:-

**AFISA MKUU MTENDAJI & KATIBU WA UDHAMINI**
**Hazina ya Pensheni ya Kenya Power,**
**Stima Plaza Annex, Barabara ya Kolobot, Parklands**
**P.O Box 1548 - 00600**
**Nairobi, Kenya.**

**na kuwekwa kwenye kisanduku cha Zabuni kwenye Orofa ya chini, Stima Plaza Annex karibu na Lift Lobby**

Ili kupokelewa kabla au kabla ya tarehe za kufunga zilizoonyeshwa hapo juu. Zabuni zitafunguliwa mara moja mbele ya Mzabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria katika Kenya Power Pension Fund, katika orofa ya chini ya Stima Plaza Annex, Barabara ya Kolobot, Parklands, Nairobi.

Isipokuwa kwa kujibu ombi la KPPF la ufafanuzi, wazabuni hawatawasiliana au kujadili kipengele chochote cha zabuni na KPPF baada ya tarehe ya kufunga zabuni na kabla ya kupokea arifa ya utoaji wa zabuni au barua za masikitiko, kama inavyotumika. Mawasiliano yoyote kama hayo yatapelekea mzabuni kutostahiki.

**CEO & KATIBU WA UDHAMINI**

KENYA VISION 2030

" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"




# Mpango mpya wa KFCB wa kuwezesha walezi na ujuzi wa malezi dijitali

NA MUTISO MBITHI (MYGOV)

Bodi ya Kutathmini Filamu ya Kenya (KFCB) imeshirikiana na Netflix, Google, Tik Tok na wadau wengine kuanzisha Mpango wa Elimu ya Malezi Dijitali kwa wazazi (PaDiL).

Mpango huo mpya utawapa wazazi na walezi ujuzi unaohitajika kuwaongoza katika matumizi salama ya majukwaa ya dijitali.

Mpango wa PaDiL utahamasisha wazazi na walezi kuhusu athari za maudhui na tekinolojia ibuka kwa watoto.

Akizungumza katika uzinduzi katika hoteli moja ya Nairobi, Katibu wa Idara ya Masuala ya Vijana na Sanaa, Bw Ismail Maalim Madey alishukuru Netflix na wadau wengine kwa kushirikiana na KFCB kuanzisha mpango mpya wa PaDiL. Katibu Madey pia alishukuru washirika kwa ushirikiano wao na serikali kupitia mashirika kadhaa kuendeleza ajenda ya kulinda watoto mtandaoni na kuhakikisha usawazishaji kati ya biashara na usalama wa watoto katika tekinolojia ya dijitali.

> Utafiti umeonyesha intaneti hufanikisha mafunzo kwa njia ipasavyo- Madey

" Huu ni mpango mzuri ikizingatiwa kwamba Kenya ina intaneti kote na ni miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa upatikanaji wa intaneti Afrika. Kutokana na hilo, matumizi ya ICT, ikiwemo mitandao ya kijamii, yamekuwa kote nchini hasa miongoni mwa vijana na watoto na kwa hivyo ninafuraha kusema uzinduzi huu umepangwa kusadifiana na maadhimisho ya 10 ya Siku ya Usalama wa Intaneti chini ya mada: 'Pamoja kwa intaneti salama," alisema Katibu.

Aliongeza kuwa serikali inachukuliwa ulinzi wa watoto kama moja ya vipaumbele vyake inavyosema Ibara 53 ya Katiba inayotambua haki ya watoto kupatiwa ulinzi dhidi ya dhuluma, kupuuzwa, tamaduni hatari, aina zote za ghasia na kutendewa maovu." Kuendelea kwa serikali kutekeleza sheria ya watoto ni dhihirisho ya kujitolea kwetu kuhakikisha maslahi ya watoto," aliongeza Katibu.

"Utafiti umeonyesha kuwa upatikanaji wa intaneti miongoni mwa watoto unawafaidi kimasomo. Katika kiwango kikubwa, upatikanaji wa intaneti ya kasi ya juu umegunduliwa kuchangia maendeleo ya uchumi na kuimarisha viwango vya maisha vya raia, wakiwemo watoto," alisema.Kaimu Afisa Mkuu Mtendaji wa KFCB Christopher Wambua alisema kwamba wazazi na walezi ni muhimu kwa watoto na hivyo basi kuna haja ya kuwapa ujuzi wanaoweza kutumia kusaidia watoto wanaowalea kutumia dijitali salama.

REPUBLIC OF KENYA

MINISTRY OF DEFENCE

NOTICE TO THE PUBLIC

SUCCESSFUL CANDIDATES FOR VARIOUS POSTS (CIVILIAN STAFF)

Following the interviews of various cadres that were conducted by the Ministry from 5th September, 2022 to 7th October, 2022, Successful candidates are asked to check their names on the Ministry's website www.mod.go.ke and on official social media pages.

DIRECTOR
HRM&D

KENYA VISION 2030

www.wasreb.go.ke

REPUBLIC OF KENYA

WASREB
Water Services Regulatory Board

WATER ACT 2016 Section 139

TANGAZO LA UMMA

MKUTANO WA UMMA KWA LESENI YA KUENDELEA KAMA MTOA HUDUMA YA MAJI KWA MFUMO WA HUDUMA YA MAJI YA BWAWA LA KARIMENU II

Bodi ya Udhibiti wa Huduma za Maji (WASREB) imepokea maombi kutoka kwa Mamlaka ya Kustawisha Kazi za Maji ya Athi (AWWDA) kuhudumu kama mtoa huduma wa maji kwa wingi ili kusambaza maji kwa watoa huduma za maji katika Kaunti za Kiambu na Nairobi.

Maombi ya leseni yamefanywa kwa mujibu wa Sheria ya Maji ya mwaka 2016 (Kifungu cha 68 (b)) kuhusu mamlaka na kazi za Wakala wa Maendeleo ya Ujenzi wa Maji kwa; ***"endesha mitambo ya maji na kutoa huduma za maji kama mtoa huduma ya maji, hadi wakati ambapo jukumu la uendeshaji na usimamizi wa mifereji ya maji likabidhiwe kwa serikali ya kaunti, kamati ya pamoja, mamlaka ya serikali za kaunti au mtoaji huduma za maji ndani ya eneo lake mamlaka au usambazaji wa mitambo ya maji iko'.***

Kwa mujibu wa Sheria ya Maji ya 2016 Kifungu cha 139 kuhusu hitaji la lazima la kushauriana na umma na mamlaka ya WASREB chini ya Kifungu cha 71(a) cha Sheria ya Maji ya 2016 - ***ulinzi wa maslahi na haki za watumiaji katika utoaji wa huduma za maji',*** tungependa kushauri kwamba mkutano wa mashauriano ya umma kwa ajili ya uendeshaji wa mfumo wa Ugavi wa Maji kwa Wingi wa Karimenu II, pamoja na, ushuru wa maji kwa wingi, utafanyika katika eneo lililotajwa hapa chini ili kupata maswala ya wadau kuhusu huduma zinazotolewa, masharti ya leseni, kiwango cha ushuru wa wingi na mapendekezo ya maendeleo ya huduma kwenda mbele.

| MTOA HUDUMA WA MAJI KWA WINGI | KAUNTI ZA KUHUDUMU | ENEO | TAREHE NA WAKATI |
|---|---|---|---|
| Athi Water Works Development Agency | Kiambu na Nairobi | Rainbow Hotel, Ruiru Town | Jumatano Machi 8, 2023<br>saa10.00 asubuhi |

Wadau wawe wameketi kabla ya saa 10.00 asubuhi. Utambulisho wa kibinafsi wa washikadau utahitajika. Wadau kutoka kaunti zilizoathiriwa (Nairobi na Kiambu) wanaalikwa kuwasilisha mawasilisho ya mdomo na maandishi na kuuliza maswali yoyote ambayo yanaweza kuhusiana na utoaji wa huduma za maji katika maeneo yao.
Maelezo kuhusu kiwango cha ushuru kwa wingi yanaweza kupatikana katika www.wasreb.go.ke.
Maoni kuhusu ombi yatatumwa kwa barua pepe kwa info@wasreb.go.ke au kutuma kwa nakala ngumu kwa:

**Afisa Mkuu Mtendaji,**
**Bodi ya Udhibiti wa Huduma za Maji,**
**Jengo la NHIF la Orofa ya 5,**
**Barabara ya Ngong,**
**P.O Box 41621 -00100, NAIROBI.**

Tarehe ya mwisho ya kupokea maoni ni siku 30 baada ya kuchapishwa kwa notisi hii.

AFISA MKUU MTENDAJI
BODI YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI

KENYA VISION 2030

*Water Services for All*

KETRACO
Kenya Electricity Transmission Company Limited
"Building a World Class National Grid"

NAFASI ZA KAZI

**UTANGULIZI**

Kampuni ya Kusambaza Umeme Kenya (KETRACO) ni shirika linalomilikiwa na serikali kwa 100%. lililoanzishwa tarehe 2 Desemba, 2008 chini ya Sheria ya Kampuni, Sura ya 486 kama Shirika la Serikali kwa mujibu wa Waraka wa Kipindi Na. 4 wa 2004 kuhusu Nishati. Majukumu ya Kampuni ni kupanga, kubuni, kujenga, kumiliki, kuendesha na kudumisha gridi ya usambazaji wa umeme wa msongo wa juu na viunganishi vya umeme vya kikanda.

Maono ya KETRACO ni kuwa kampuni ya kiwango cha kimataifa ya usambazaji umeme na kiunganishi kinachoongoza barani Afrika. Dhamira ya Kampuni ni kutoa usambazaji wa umeme wa kutegemewa, unaofaa na kukuza biashara ya kawi kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Kwa hili, Kampuni inakaribisha maombi kutoka kwa watu wanaofaa kujaza nafasi zifuatazo:

| No | Nafasi | Daraja | Idadi | Mfumo | Namba ya Marejeleo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Meneja Mkuu, Uendeshaji na Matengenezo ya Mfumo | KET 3 | 1 | Mkataba | KET/5/1C/40/15- B/VOL II |
| 2. | Meneja, Uhakikisho wa Ubora na Usimamizi wa Hatari | KET 4 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/157-B/Vol I |
| 3. | Meneja, Mikataba ya Huduma za Kisheria na Utawala | KET 4 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/148 -B/VOL I |
| 4. | Mchambuzi Biashara na Malipo ya HCM | KET 6 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/158-B/Vol I |
| 5. | Afisa Usalama -Uchunguzi | KET 6 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/145-B/Vol I |
| 6. | Afisa wa Bima | KET 6 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/144-B/Vol I |
| 7. | Afisa Sheria, Huduma za Uzingatiaji | KET 7 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/156-B/VOL |
| 8. | Mhandisi Mhitimu wa Mafunzo-Umeme | KET 7 | 20 | P&P | KET/5/1C/40/63-B/Vol IV |
| 9. | Waendeshaji wa Kituo kidogo - Mafundi | KET 8 | 15 | P&P | KET/5/1C/40/93-B/Vol III |

Maelezo ya kina ya kazi, vipimo na mahitaji mengine yamewekwa kwenye tovuti yetu **www.ketraco.co.ke**.

**KUMBUKA:**

i. Uteuzi wa nafasi Na. 1 ni kwa masharti ya mkataba wa miaka mitano (5) na unaweza kurejeshwa kulingana na utendaji;
ii. Maombi yote kutoka kwa wagombea wanaovutiwa na waliohitimu lazima yawasilishwe kwa njia ya mtandao.
iii. Tutawasiliana na wagombea watakaoorodheshwa pekee.
iv. KETRACO haitozi ada yoyote kwa kutuma maombi, usindikaji, usaili au ada nyingine yoyote kuhusiana na mchakato wetu wa kuajiri.
v. KETRACO ni mwajiri anayetoa fursa sawa aliyejitolea kujumuisha jinsia na ulemavu. Watu wenye Ulemavu wanahimizwa kutuma maombi.

Waombaji walio na nia na waliotimiza masharti yanayohitajika wanapaswa kutuma maombi yao kwa uwazi yakionyesha nafasi iliyoombwa na Namba ya Kumbukumbu ya Nafasi. kupitia **kiungo cha kazi** kilichowekwa kwenye tovuti ya KETRACO na kuambatanisha nakala za vyeti na nakala, wasifu wa sasa na ushuhuda mwingine wowote unaofaa, mawasiliano ya simu, anwani ya barua pepe na wadhamini watatu (3) na maelezo ya mawasiliano yao ili kufikia anwani iliyo hapa chini kwa kufikia **Jumanne, tarehe 28 Februari 2023 saa 5:00PM EAT.**






REPUBLIC OF KENYA

## KAMPUNI YA KENYA PIPELINE

***Africa's Premier Oil & Gas Company***

KPC

**KENPIPE PLAZA,
SEKONDI ROAD,
OFF NANYUKI ROAD,
INDUSTRIAL AREA,
NAIROBI, KENYA.
P.O.Box 73442 - 00200,
TELEPHONE: 254-20-2606500-4
MOBILE: 0722 207 678/9
0734 333 217/219/234/226
E-mail: Info@kpc.co.ke**

## MWALIKO WA ZABUNI

Kampuni ya Kenya Pipeline inaalika zabuni kutoka kwa wagombeaji wanaostahiki kwa yafuatayo::

| NO. | KUMBUKUMBU NA MAELEZO | DHAMANA | KUZURU ENEO | KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|
| | **ZABUNI WAZI KITAIFA** | | | |
| 1. | **KPC/PU/OT – 104/AIRWING/NBI/22 - 23**<br>Zabuni ya Ukarabati na Matengenezo ya Helikopta | Kes.200,000.00 | N/A | 08-03-2023 |
| 2. | **KPC/PU/OT – 105/AIRWING/NBI/22 - 23**<br>Zabuni ya Utoaji wa Huduma ya Hangarage | Kes.100,000.00 | N/A | 08-03-2023 |
| 3. | **KPC/PU/OT – 259/I&C/NBI/22 - 23**<br>Zabuni ya Usambazaji, Usakinishaji na Uagizo wa Kitambua Kiolesura, Uboreshaji wa Banda la Nje na Makubaliano ya Kiwango cha Huduma kwa PS25 - Nakuru, PS27 Eldoret na PS28 - Kisumu | Kes.200,000.00 | 22-02-2023 hadi 24-02-2023 | 08-03-2023 |
| 4. | **KPC/PU/OT – 258/CORR/NBI/22 - 23** Zabuni ya Ugavi wa Vipuri vya Ulinzi wa Cathodic kwa Matengenezo ya Bomb**a** | Kes.100,000.00 | N/A | 08-03-2023 |
| | Nyaraka za Zabuni zinaweza kutazamwa na kupakuliwa kutoka kwa tovuti **www.kpc.co.ke** bila gharama yoyote. Wazabuni watahitajika kusajili kampuni zao kwenye tovuti ya KPC SRM na kutuma maswali **PEKEE** kwa **opentender@kpc.co.ke**. Zaidi ya hayo, nyongeza zote zitabandikwa kwa wazabuni hao ambao wanaonyesha nia yao ya kushiriki kupitia tovuti ya SRM.<br><br>**Hakuna anwani zingine za barua pepe zitatumika na KPC haitawajibika ikiwa wazabuni watachagua kutuma hoja zao kwa anwani zingine za barua pepe.** | | | |
| | **MKATABA WA MFUMO** | | | |
| 5. | **KPC/PU/FW – 133/I&C//NBI/22 – 23**<br>Zabuni ya Mkataba wa Mfumo wa Mtandao wa Redio wa VHF | N/A | N/A | 09-03-2023 |
| 6. | **KPC/PU/FW – 153/I&C/NBI/22 – 23**<br>Zabuni ya Mkataba wa Mfumo wa Utoaji wa Mfumo wa Mawasiliano wa 10G | N/A | N/A | 09-03-2023 |
| | Nyaraka za Zabuni zinaweza kutazamwa na kupakuliwa kutoka kwa tovuti **www.kpc.co.ke** bila gharama yoyote. Wazabuni watahitajika kusajili kampuni zao kwenye tovuti ya KPC SRM na kutuma maswali **PEKEE** kwa **technicalprocurement@kpc.co.ke** Zaidi ya hayo, nyongeza zote zitabandikwa kwa wazabuni hao ambao wanaonyesha nia yao ya kushiriki kupitia tovuti ya SRM.<br><br>**Hakuna anwani zingine za barua pepe zitatumika na KPC haitawajibika ikiwa wazabuni watachagua kutuma hoja zao kwa anwani zingine za barua pepe.** | | | |
| | **KUMBUKA: Wazabuni ambao hawajasajiliwa kwenye Mfumo wa KPC SRM wanapaswa kujisajili kwanza kwa kutumia kiungo hiki https://e-procurement.kpc.co.ke/irj/portal**<br>**Mafunzo ya zabuni na miongozo ya mafunzo inapatikana kwenye tovuti ya KPC www.kpc.co.ke/Tenders-Miongozo ya Mtumiaji ya SRM** | | | |
| | Wazabuni wote watahitajika kuwasilisha zabuni hizo mtandaoni kupitia Tovuti ya SRM **https://e-procurement.kpc.co.ke/irj/portal** na ni **LAZIMA** hati zote zipakiwe kwenye **KISANDUKU CHA USHIRIKA.** Wazabuni hawataambatanisha hati zao kwenye kichupo kingine chochote cha tovuti. Itapokelewa **tarehe iliyoonyeshwa ya kufunga saa 10.00 asubuhi** au kabla. | | | |
| | **USAJILI** | | | |
| 7. | **KPC/PU/REG – 049/FINANCE/NBI/22 – 23** Usajili wa Wasambazaji kwa Utoaji wa Huduma za Ushauri wa Ushuru kwa Kipindi cha Miaka Miwili. | N/A | N/A | 10-03-2023 |
| | Nyaraka za Zabuni zinaweza kutazamwa na kupakuliwa kutoka kwa tovuti **www.kpc.co.ke** bila gharama yoyote. Wazabuni watahitajika kusajili kampuni zao kwenye tovuti ya KPC SRM na kutuma maswali PEKEE kwa **technicalprocurement@kpc.co.ke.** Zaidi ya hayo, nyongeza zote zitabandikwa kwa wazabuni hao ambao wanaonyesha nia yao ya kushiriki kupitia tovuti ya SRM.<br><br>**Hakuna anwani zingine za barua pepe zitatumika na KPC haitawajibika ikiwa wazabuni watachagua kutuma hoja zao kwa anwani zingine za barua pepe.**<br><br>Wazabuni wote watahitajika kuwasilisha zabuni kupitia kisanduku cha e-tender: **e-tenderbox@kpc.co.ke** ipokewe kabla au kabla ya tarehe iliyoonyeshwa ya kufunga **saa 10.00 asubuhi.** | | | |

**(HAKUNA ZABUNI ZITAKUBALIWA KWENYE SANDUKU LA ZABUNI ISIPOKUWA DHAMANA HALISI YA ZABUNI)**
**Ufunguzi wa zabuni utafanyika saa 10.30 asubuhi.**

**KAIMU MENEJA MKUU (MFUMO WA USAMBAZAJI)**
**KWA: MKURUGENZI MKUU**

KENYA VISION 2030

TECHNICAL UNIVERSITY OF MOMBASA

## CHUO CHA KIUFUNDI CHA MOMBASA

**P.O. BOX 90420-80100 Mombasa, KENYA**
**Simu: 0733955377: B/Pepe: procurement@tum.ac.ke**

## TANGAZO LA KAZI

**WASIFU WA TAASISI**

Chuo Kikuu cha Kiufundi cha Mombasa (TUM) ni Chuo Kikuu cha Ufundi cha Umma nchini Kenya kilicho katika Kaunti ya Mombasa, chenye wanafunzi 18,622 na wafanyikazi 594. Chuo kinalenga kuongeza programu za kitaaluma, uandikishaji wa wanafunzi na uwezo wa nguvukazi ili kufikia dira yake ya kimkakati ya kuwa Chuo Kikuu cha Ubora wa Kimataifa katika Kuendeleza Sayansi na Teknolojia ya Maarifa.

Ili kutekeleza maono yake, dhamira na malengo ya kimkakati, Chuo kinakusudia kuajiri watu wabunifu walio na viwango vya juu vya uadilifu wa kibinafsi na kitaaluma kwa nyadhifa zifuatazo.

| S/No | Nafasi | Daraja | Kitengo/Shule | Idara | Nafasi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Afisa wa Ngazi ya Juu wa Mawasiliano II ***(Mkataba)*** | 12N | Usimamizi | Afisi ya Mawasiliano | 1 |
| 2. | Afisa wa Sheria III (***Kudumu na Pensheni)*** | 9N | Usimamizi | Afisi ya Sheria | 1 |
| 3. | Mhasibu Msaidizi II ***(Kudumu na Pensheni)*** | 8N | Usimamizi | Fedha | 1 |
| 4. | Mtaalamu wa Matengenezo ***(Kudumu na Pensheni)*** | 8N | Usimamizi | Matengenezo | 1 |
| 5. | Afisa Usalama na Afya Kazini II ***(Kudumu na Pensheni)*** | 9N | Usimamizi | Msajili (AP) | 1 |
| 6. | Afisa Usalama na Afya Kazini II ***(Kudumu na Pensheni)*** | 5N | Masomo, Utafiti na Ugani | Mkuu wa Wanafunzi | 1 |
| 7. | Msaidizi wa Michezo I (Bewa la Kwale) ***(Kudumu na Pensheni)*** | 7N | Masomo, Utafiti na Ugan | Mkuu wa Wanafunzi | 1 |
| 8. | Mhadhiri/Mtafiti Mshirika (Famasia) ***(Kudumu na Pensheni)*** | 12A | Shule ya Sayansi Tekelezi na Afya | Sayansi ya Tiba | 1 |
| 9. | Mhadhiri/Mtafiti (Maabara ya Matibabu) ***(Kudumu na Pensheni)*** | 12A | Shule ya Sayansi Tekelezi na Afya | Sayansi ya Tiba | 2 |
| 10. | Mhadhiri/Mtafiti Mshirika (Afya ya Umma***) (Kudumu na Pensheni)*** | 12A | Shule ya Sayansi Tekelezi na Afya | Sayansi ya Mazingira na Afya | 3 |
| 11. | Mhadhiri / Mtafiti Mshirika-Usimamizi wa Ujenzi ***(Kudumu na Pensheni)*** | 12A | Uhandisi na Teknolojia | Ujenzi na Uhandisi wa Ujenzi | 1 |
| 12. | Mhadhiri Mkuu - Ujasiriamali ***(Kudumu na Pensheni)*** | 13A | Shule ya Biashara | Usimamizi wa Biashara | 1 |
| 13. | Mhadhiri Mkuu Sayansi ya Masuala ya Maktaba ***(Kudumu na Pensheni)*** | 13A | Shule ya Sanaa na Sayansi ya Jamii | Sayansi ya Jamii | 1 |

Waombaji wanaovutiwa wanapaswa kupata tangazo na maelezo ya kina ya mahitaji ya nafasi zilizotumwa kwenye Tovuti ya Chuo Kikuu (**www.tum.ac.ke**)

**MWONGOZO WA MAOMBI**

1. Maombi lazima yajumuishe Wasifukazi (CV) iliyosasishwa, inayotoa maelezo ya umri, taaluma na sifa za kitaaluma, uzoefu wa kazi, nafasi ya sasa na mshahara, anwani ya barua pepe, simu, jina na mawasiliano ya waamuzi watatu ambao wana ufahamu kuhusu uwezo wa mwombaji, nakala ya Kitambulisho cha Taifa, nakala za vyeti na ushuhuda husika.
2. Waombaji walio na Sifa za Kielimu za kigeni LAZIMA wawasilishe Cheti cha Kutambuliwa kutoka Tume ya Elimu ya Vyuo Vikuu (CUE).
3. Maelezo ya vyeti vya taaluma na taaluma ambayo hayakupatikana kwa kufungwa kwa tangazo hayatazingatiwa.
4. Baada ya kutoa ajira watahiniwa waliofaulu watahitajika kutoa vyeti halali vya kibali kutoka kwa Mashirika yafuatayo:
   a. Mamlaka ya Kukusanya Ushuru Kenya.
   b. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.
   c. Tume ya Maadili na Kupambana na Rushwa.
   d. Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai
   e. Ofisi Iliyosajiliwa ya Marejeleo ya Mikopo.
5. Waombaji walioteuliwa na waliofaulu pekee ndio tutakaowasiliana nao

Waombaji walio na nia wanapaswa kutuma nakala sita (6) za maombi yao kwa nafasi zilizo hapo juu. Maombi yenye taarifa za uongo yataondolewa.

Barua za maombi na mapendekezo kutoka kwa wadhamini zinapaswa kutumwa kwa;

**Naibu Chansela**
**Chuo kikuu cha Kiufundi cha Mombasa**
**P.O Box 90420-80100**

Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ni tarehe **28 Februari, 2023.** Maombi yatakayopokelewa baada ya tarehe hii hayatazingatiwa. Tafadhali nukuu nambari ya kumbukumbu katika ombi lako.

***Chuo kikuu cha kiufundi cha Mombasa ni mwajiri anayetoa fursa sawa. Wanawake, watu wanaoishi na ulemavu na makundi yaliyotengwa wanahimizwa kutuma maombi.***

***Chuo kikuu hakiulizi ada yoyote kutoka kwa waombaji.***

**TUM is ISO 9001:2015 Certified**

**A University of global excellence in advancing Knowledge, Science and Technology**

KOMESHA COVID-19

" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"




# Watetezi wa haki za watoto watatizika kusaidia wanaodhulumiwa

**NA GEORGE AGIMBA (KNA)**

Mashirika yanayoendesha kampeni ya kuokoa watoto wanaodhulumiwa kama vile kupigwa, kutumiwa kwa vitendo vya ngono, ukeketaji wa wanawake (FGM), mihandarati na kufanyishwa kazi, wamebaini kuwa kuwaokoa kutoka maovu hayo ni sehemu tu ya vita hivyo.

Kuhakikisha kuwa wanaepuka vitendo hivyo vibaya ni suala tofauti kabisa.

"Juhudi zote, kwa mfano, za kuangamiza matumizi ya watoto katika vitendo vya ngono havitafaulu hadi pale umakinivu utaelekezwa kwa kusaidia waathiriwa kupona," asema Bw Tobias Marwa wa Centre for Assault and Recovery (CARE), tawi la Migori. Ilhali, kulingana na Bw Marwa, hakuna mipango ya kutosha inayowekwa na serikali kusaidia waathiriwa wanaodhulumiwa kupona kutokana na uharibifu wanaofanyiwa na wanaowatesa.



**Watoto wakusanya changarawe mtoni,shughuli ambayo imetambuliwa kama udhalimu mkubwa wa haki za watoto.**

Ingawa Afisa wa Watoto wa Kaunti Ndogo ya Kuria Magharibi, Bw James Omondi anasisitiza kujitolea kwa serikali kupiga vita kutumiwa kwa watoto kingono, ndoa za mapema, FGM, mihandarati na aina zote za ghasia za jinsia dhidi ya watoto katika Migori na nchi nzima, mashirika ya mashinani yanatilia shaka iwapo serikali imetoa usaidizi zaidi ya maneno tu.

Bw Omondi, katika mahojiano na Kenya News Agency majuzi, alisikitikia kuendelea kuongezeka kwa ukiukaji wa haki za watoto kunakoripotiwa katika eneo hilo na katika nchi kwa jumula, akisema nyingi ya visa hivi hutokea nyumbani au vinatekelezwa na watu wanaofahamika na waathiriwa.

# National Environment Management Authority

nema
mazingira yetu | uhai wetu | wajibu wetu

**Popo Road, off Mombasa Road P.O.BOX 67839-00200, Nairobi, Kenya,**
**Tel: 0724253398, 0735013046 E-mail: dgnema@nema.go.ke Website: www.nema.go.ke**

Wadau katika sekta ya afya wameunda mfumo wa kibaiyometriki wa usimamizi wa chanjo ya watoto wapya wanaozaliwa nchini Kenya.

Uthibitishaji wa mfumo huo mpya unaendelea katika Taasisi ya Utafiti wa Matibabu Kenya (KEMRI) huku majaribio yaliyoanza Septemba mwaka jana yakiendelea katika Hospitali ya Kaunti Ndogo ya Kinango, Kwale, na matokeo ya mwanzo yakisemekana kuwa ya kutia moyo.

Ubunifu wa kisayansi unafanywa na KEMRI, NEC Corporation na Chuo Kikuu cha Nagasaki, Japan. Katika taarifa kwa vyombo vya habari, Kaimu Mkurugenzi wa KEMRI Prof. Sam Kariuki alisema mfumo huo wa dijitali utasimamia vyema historia ya chanjo na kupangia ijayo kwa kutumia alama za vidole kutambua watoto wachanga na sauti za walezi wao.

"Tekinolojia hii inaashiria mara ya kwanza ambayo kutambuliwa kibaiyometriki kunatumiwa kutambua watoto wachanga wakati wa kupata chanjo, ikiwemo punde tu baada ya kuzaliwa," akasema.

Alisema kufikia Novemba 2022, data kutoka walezi na watoto wachanga zaidi ya 300 zilikuwa zimesajiliwa, ikiwemo historia ya chanjo ya zaidi ya watoto wachanga 150. Prof Kariuki alisema tekinolojia hiyo mpya inaunganisha kutumia alama za vidole kutambua watoto na kutambua sauti ya walezi sio tu kuthibitisha lakini pia kusimamia vyema historia zao za chanjo na wakati wa kuzipata.

Mkurugenzi huyo wa KEMRI alisema tekinolojia inainua utekelezaji wa chanjo zinazofaa kwa watoto wanaozaliwa katika miezi 24 ya maisha yao.

> Kutambua watoto wachanga kwa vidole sasa kunawezekana- Kariuki

Kuendelea mbele, majaribio yataanza katika hospitali kadhaa, yakilenga kuanzishwa kote Kenya kufikia mwisho wa 2023, na maeneo mengine ya ulimwengu baadaye, alisema. "Tunafuraha kwamba KEMRI, pamoja na washirika wake wanaongoza utafiti huu wa kipekee ambao unatarajiwa kuinua sera ya upatikanaji wa matokeo bora ya afya na Afya kwa Wote," alisema.

"Niko na furaha kutangaza kuwa kifaa hili kitathibitishwa na watafiti wa KEMRI kwa ushirikiano na hospitali ya kaunti ndogo ya Kwale, NEC Corporation na Chuo Kikuu cha Nagasaki," Kariuki aliongeza.

"Ninatarajia mfumo huu wa usimamizi wa chanjo utatoa utambuzi sahihi wa mama na watoto Kenya," alisema.

REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO YA UCHUMI

### MWALIKO WA ZABUNI

**UNUNUZI WA VIFAA VYA HYPERION / BAJETI YA MFUMO**
**ZABUNI NAMBA. TNT/016/2022-2023**

Wizara ya Fedha inakaribisha Zabuni zilizofungwa kutoka kwa Wagombea wanaostahiki kwa **Ununuzi wa Vifaa vya Mfumo wa Hyperion / Bajeti.**

Kongamano la **Lazima** la Matayarisho ya Kabla ya Zabuni litafanyika pamoja na Wazabuni wanaovutiwa mnamo **Jumanne tarehe 21 Februari, 2023 saa 1000, Saa za Kenya** kupitia mkutano wa mtandaoni. Mialiko itatumwa kwa wazabuni wote wanaovutiwa ambao watawasilisha barua pepe zao kwa procurement@treasury.go.ke kabla ya **Saa 10.00, Saa za Kenya** mnamo **Jumanne tarehe 21 Februari, 2023**.

Seti kamili ya Hati za Zabuni inaweza kupakuliwa na wagombeaji wanaovutiwa na wanaostahiki ***Bila Malipo*** katika http://treasury.go.ke au www.tenders.go.ke. Wale wanaopakua hati kutoka kwa tovuti lazima watume maelezo yao mara moja kwa ajili ya kurekodiwa na ufafanuzi wowote zaidi na nyongeza kwa procurement@treasury.go.ke. Nyaraka za Zabuni zilizokamilishwa, ***"Halisi"*** na "***Nakala"***, zilizoambatanishwa katika bahasha iliyofungwa na kuwekwa Nambari ya Zabuni, zitatumwa kwa: -

**Katibu wa Wizara,**
**Wizara ya Fedha,**
**P.O. Box 30007 00100 Nairobi**

na kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni lililo katika **Wizara ya Fedha, Jengo la Treasury, Orofa ya 6, Barabara ya Harambee, Nairobi**, ili ipokewe mnamo au kabla ya **Jumanne tarehe 21 Februari, 2023 saa 11.00 asubuhi** kwa **Saa za Kenya.**

**Hati zote za Zabuni lazima ziwe na mpangilio / kuwekwa nambari kwenye kurasa.**

Zabuni zote lazima ziambatane na Dhamana ya Benki ya **Shilingi za Kenya Laki Tisa Pekee (Ksh. 900,000.00)** kutoka kwa Benki Inayoaminika nchini Kenya inayotumika kwa siku 30 zaidi ya muda wa Uhalali wa Zabuni.

Zabuni zitafunguliwa mara moja mbele ya Wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria ufunguzi huo katika **Wizara ya Fedha, Jengo la Treasury, Barabara ya Harambee, Nairobi, Orofa ya 6, Chumba cha Mikutano Nambari 603 Jumanne tarehe 21 Februari, 2023 saa 11.00 asubuhi Saa za Kenya.**

**MKUU, HUDUMA ZA MFUMO WA USAMBAZAJI**
**KWA: KATIBU/ WIZARA YA FEDHA**

KENYA VISION 2030

KETRACO
Kenya Electricity Transmission Company Limited
"Building a World Class National Grid"

## NOTISI YA TENDA

Kenya Electricity Transmission Company Limited (KETRACO) ni Shirika la Kiserikali linalomilikiwa na Serikali. Jukumu la Kampuni ni kupanga, kuunda, kujenga, kumiliki, kusimamia na kutunza nyaya za kusafirisha kiwango kikubwa cha umme na vituo vingine unganishi vya umeme.

KETRACO inaalika maombi kutoka kwa taasisi zilizohitimu kutoa huduma zifuatazo.

| S/no | Maelezo ya Tenda | Nambari ya Marejeo | Tarehe ya Mwisho |
|---|---|---|---|
| 1. | Utoaji wa Huduma za Kutunza Helikopta | KETRACO-PT-003-2023 | Machi 1, 2023 saa 4.00 asubuhi |
| 2. | Ununuzi na kuleta viyoyozi (Air Conditioners) Kubadilisha vifaa vya AC | KETRACO-PT-004-2023 | Machi 2, 2023 saa 4.00 asubuhi |
| 3. | Kununua mafuta ya Jet A-1 kwa Helikopta ya KETRACO | KETRACO-PT-005-2023 | Machi 1, 2023 saa 5.00 asubuhi |

Tenda za KETRACO zinaendeshwa kwenye jukwaa la SAP ARIBA na hivyo stakabadhi zote za tenda zinazoelezea kuhusu mahitaji zinaweza kupatikana kwenye lango kuu la tenda la KETRACO ambalo liko kwenye wavuti wa KETRACO (***www.ketraco.co.ke***) kuanzia Jumanne **Februari 14, 2023.**

Maswali, ufafanuzi, maelezo zaidi yaweza kutumwa kwa ***pkubasu@ketraco.co.ke*** na ***lswaleh@ketraco.co.ke.*** Stakabadhi zote za tenda zinapasa kutumwa kwa njia ya kielektroniki kupitia jukwaa la SAP ARIBA mnamo au kabla ya siku ya mwisho.

Tenda zitafunguliwa kielektroniki papo hapo mbele ya waliotuma maombi au wawakilishi wao ambao wataamua kuhudhuria katika afisi za KETRACO Supply Chain Management katika KAWI House, South C, Nairobi.

**SENIOR MANAGER, SUPPLY CHAIN MANAGEMENT**
**KWA NIABA YA KAIMU MKURUGENZI MKUU**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

COMPETITION AUTHORITY OF KENYA
Creating efficient markets for consumers

## NAFASI ZA KAZI

Competition Authority of Kenya (Authority)ni shirika la kiserikali lililoanzishwa chini ya Kifungu cha Sheria Competition Act No.12 ya 2010. CAK ina mamlaka ya kuendeleza na kudumisha ushindani na kutetea wanunuzi kutokana na ulaghai sokoni.

CAK inaendesha mpango wa mwaka mmoja wa mafunzo kazini kwa wanaohitimu kutoka vyuo vikuu. Lengo la mpango huo ni kuwaandaa wanafuzu kujiunga na maeneo ya kazi katika mazingira halisi ili kuimarisha ujuzi wao kazini na uwezo wao wa kuajiriwa.

Shirika hili linaliika wale waliohitimu kutuma maombi kujiunga na mpango huo wa mafunzo kazini katika mwaka wa 2023 katika nyanja zifuatazo:

| Nyanja | Idadi ya nafasi | Marejeleo ya kazi |
|---|---|---|
| Utekelezaji na uzingatiaji sheria | 1 | CAK/01.02/2023 |
| Kutetea wanunuzi | 1 | CAK/02.02/2023 |
| Katibu wa Kampuni na Huduma za Sheria | 1 | CAK/03.02/2023 |
| Hazina | 1 | CAK/04.02/2023 |
| Masuala ya Wafanyakazi na Usimamizi | 1 | CAK/05.02/2023 |

Wanaopenda kutuma maombi wanaweza kupata maelezo kamili kuhusu mpango huu na yale yanayohitajika kwa kila nafasi kutoka kwa wavuti wa CAK **www.cak.go.ke** na wale wanaotimiza mahitaji yaliyowekwa wanashauriwa kuwasilisha maombi yao kwa: baruapepe: **recruitment@cak.go.ke**

***Ni waliohitimu tu tutakaowasiliana nao***

***Competition Authority of Kenya ni "Mwajiri anayetoa nafasi sawa kwa wote"***
***Kampeni ya aina yoyote ya kutafuta kazi itafanya ombi lako litupwe nje***

ISO 9001:2015 CERTIFIED




# Kampuni yatumia masalia ya miwa kuunda vidonge kutumika kama kawi

**NA MOSES WEKESA**

Kampuni ya humu nchini, Powerspot Pelletizers, imejenga kiwanda cha kutengeneza vidonge kutoka masalia ya miwa kaunti ya Kakamega.

Vidonge hivyo ambavyo havitoi moshi vinatumiwa kama kawi katika meko na vinaweza kutumiwa badala ya makaa na kuni na hivyo basi kupunguza ukataji wa miti.

Kwa wakati huu kampuni hiyo inatengeneza tani 100 za vidonge hivyo kutoka karibu tani 200 za masalia ya miwa.

Afisa Mkuu Mtendaji wa kampuni hiyo Alfonso Acebal anasema kwamba mipango inaendelea ya kujenga kiwanda kama hicho kilicho na uwezo mkubwa wa kutengeneza zaidi ya tani 2000 za vidonge kutoka tani zipatazo 4500 hadi 5000 za masalia ya miwa.

Anasema kwamba mali ghafi hiyo ambayo ni masalia ya miwa inapatikana kwa wingi na kiwanda hicho cha pili kitakapojengwa, kitakuwa afueni kubwa kwa kampuni za miwa ambazo huwa zinatupa masalia ya miwa yasiyotumika.

Anasema kwamba kampuni hiyo pia imetengeneza meko ambayo awali yalitumia vidonge kutoka vumbi ya mbao na ambayo sasa yanatumia vidonge vinavyotengenezwa kutoka masalia ya miwa. Acebal ilianzisha kampuni hiyo 2017, lakini baada ya utafiti wa kina na majaribio ambayo yalichukua muda.

> Malighafi ambayo ni masalia ya miwa yamo kwa wingi na kampuni za sukari zitapata nafuu kubwa -Acebal



**Jiko ya umemejoto inayotumia vidonge kutoa kawi pamoja na umeme tosha kuwasha Jiko na balbu pamoja na kujaza moto kwa simu.** PICHA: MOSES WEKESA, KNA

Anasema alitembelea Kakamega kuuza meko yanayotumia vidonge vya vumbi ya mbao kwa kuwa kampuni nyingi za Amerika na Ulaya hutengeneza vidonge kutoka vumbi ya mbao.

Katika ziara yake, pia alikuwa akifanya utafiti kuhusu jinsi ya kubadilisha jiko kutoa kawi kando na matumizi yake ya kimsingi ya kupikia, inaweza pia kuwasha taa, kuweka moto kwenye simu na hata vifaa vingine vya elektroniki kwa lengo la kutoa kawi maeneo ya mashambani Kenya.

Katika utafiti huo, walianzisha kiwanda cha kutumia vumbi ya mbao kutengeneza vidonge Kenya badala ya kuviagiza kutoka Amerika. Kiwanda hicho kilianzishwa lakini baada ya kuhudumu kwa muda, kilianza kupata changamoto ya kupata vumbi ya mbao kutokana uhaba wa miti na msimamo mkali wa serikali kuhusu uhifadhi wa misitu. Jamii ya eneo la Kabras tayari imekumbatia meko hayo na sasa inatumia vidonge kama chanzo cha kawi ya kupikia na kutumia tekinolojia ya meko hayo kupata stima ya vifaa vyao kama kuweka moto kwenye simu na kuwasha taa.

# Chuo Kikuu chazindua ambulensi za kisasa kuinua huduma za afya

**NA DICKSON MWITI (KNA)**

Chuo Kikuu cha Sayansi na Tekinolojia cha Meru (MUST) kimezindua ambulensi ya kisasa itakayosaidia utoaji wa huduma za afya kulingana na ajenda ya Afya kwa Wote katika kaunti hiyo.

Ambulensi hiyo imewekwa vifaa vya kisasa vya kusaidia kuokoa maisha ukiwemo mfumo ulioboreshwa wa hewa na vifaa vya ufuatiliaji, kifaa cha kusaidia moyo na kipumzi ili kuwezesha wafanyakazi wa matibabu wa chuo hicho kutoa huduma bora za afya katika eneo hilo. Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Makamu Chansela Prof Romanus Odhiambo alisema kwamba hatua ya kununua ambulensi hiyo inalandana na jukumu lao la kulinda afya na kuinua maisha ya binadamu ambayo ni muhimu kwa maendeleo endelevu.

“Kama chuo kikuu, tuko na jukumu kwa jamii yetu, nchi na ulimwengu mzima kutoa suluhu za afya. Hatuwezi kusahau shida tulizopata wakati wa janga la Covid-19 wakati watu hawakuweza kufika vituo vya afya kwa wakati; kwa kuanzisha ambulensi kama hii, matatizo kama hayo yanatatuliwa,” alisema Odhiambo.

Alisema lengo la Chuo Kikuu hicho ni kuokoa maisha ya watu wengi kwa kutoa huduma sahihi kwa wakati unaofaa, jukumu ambalo litaimarishwa na uwepo wa ambulensi hiyo.

Hii, alisema, inalandana vyema kabisa na jukumu la Chuo Kikuu hicho la kutekeleza jukumu muhimu katika afya ya jamii, nchi, na ulimwengu kwa jumla.

“Pia tumewekeza katika mifumo ya mawasiliano ili kuhakikisha ambulensi hiyo inashughulikia vyema dharura na kuwezesha way wa afya kuwasiliana na watoaji wengine wa huduma za dharura kwa wakati,” alisema Odhiambo.

# Polisi, askari akiba kusaidia KWS kutatua usumbufu wa ndovu Meru

**NA DICKSON MWITI (KNA)**

Serikali imeagiza polisi wote wa akiba na maafisa wa kawaida wa polisi kuungana na maafisa wa Shirika la Kulinda Wanyama Pori Kenya (KWS) kuzuia tishio la ndovu ambao wamesababisha uharibifu mkubwa wa mimea ya wakulima katika eneo la Kandebene, Tigania Magharibi.

Akizungumza katika mkutano wa dharura na wakulima walioathiriwa na viongozi wa Meru, Kamishna wa Kaunti ya Meru Fred Ndunga alisikitika kuwa hasara inayosababishwa na wanyama hao na akahimiza viongozi hao kuungana na kupata suluhu la kudumu kwa tatizo hilo.

“Nimetembelea mashamba mawili yaliyovamiwa na ndovu hao na nikaona uharibifu uliosababishwa. Tutajaribu mbinu zote tuwezavyo kuhakikisha wanyama hao wameondolewa eneo hili kuzuia uharibifu zaidi,” alisema Ndunga.

Alisema kwamba tangu 2015, hakujawahi kuwa na uajiri wa maafisa wa KWS licha ya wengi kustaafu na wengine kufariki jambo ambalo limesababisha upungufu wa wafanyakazi.

“Tumewasilisha suala hilo kwa wakubwa wetu na hatua zitachukuliwa hivi karibuni kumaliza upungufu huo,” alisema kamishna huyo wa kaunti. Ili suluhu la kudumu lipatikane, Ndunga aliongeza kuwa, viongozi wote kutoka kaunti hiyo na Serikali ya Kitaifa wanahitaji kuchunguza eneo hilo kubaini iwapo kunaweza kuwa na uvamizi wa njia za ndovu jambo ambalo linaweza kuwa chanzo cha tatizo hilo.

> Nimetembelea nashamba mawili yalivamiwa na ndovu na nimekerwa na uharibu waliosababisha -Ndunga

“Ndovu huwa na njia zao za kuhama ambazo hutumia kwa miaka mingi. Tunahitaji kupima eneo hili kubaini iwapo kuna watu ambao wamejenga njia za ukora, walipatiwa ardhi ndani ya njia zao na sasa wanazuia ndovu hao kuhama na hivyo basi kusababisha uharibifu eneo hili,” alisema.

Afisa wa cheo cha juu wa KWS Zainab Salim alisikitikia hatua za maafisa wa KWS kwa malalamishi ya wakazi wa eneo hilo akisema atakuwa alihakikisha Wana uhusiano mzuri na jamii siku zijazo.

“Ninachukua fursa hii kuomba msamaha kwa niaba ya maafisa, na kuwahakikishia kwamba tutafanya kila tuwezalo kuhakikisha kwamba ndovu wanaondolewa kutoka mashamba yenu,” Bi Salim alisema.

Aliongeza kwamba mchakato wa kutafuta fidia kwa waathiriwa wa uharibifu huo.unaendelea na akahimiza wote walioathiriwa kuhakikisha wanachukua fomu zao kutoka ofisi za KWS ili washughulikiwe.

REPUBLIC OF KENYA

KICC
The Kenyatta International Convention Centre
Africa's Premier Meeting Venue

## NOTISI YA TENDA

Kenyatta International Convention Centre inaalika maombi ya tenda kutoka kwa wale waliohitimu kutoa huduma zifuatazo:

| S/NO. | NAMBARI YA TENDA | MAELEZO YA TENDA | WASHIRIKI |
|---|---|---|---|
| 1. | KICC/08/2022-2024 | Utoaji wa Vifaa vya Mikutano | WOTE |
| 2. | KICC/09/2022-2024 | Utoaji wa Hema na Samani | WOTE |
| 3. | KICC/10/2022-2024 | Utoaji wa Maua na Mapambo | AGPO |
| 4. | KICC/11/2022-2024 | Utoaji wa Vifaa vya Maonyesho | WOTE |
| 5. | KICC/12/2022-2024 | Utoaji wa Vyoo vya Kuhamishwa | WOTE |

Stakabadhi zote za tenda zinaweza kupakuliwa kutoka kwa lango kuu la PPIP (**https://tenders.go.ke**) Au wavuti wa Shirika (**www.kicc.co.ke**) ***bila malipo.***

Nakala mbili za stakabadhi za tenda zilizojazwa na kuwekwakwenye bahasha ambayo imeandikwa ***“Maombi ya Tenda No..........................Maelezo ya Tenda...............”*** zinapasa kutumwa kwa:

**Afisa Mkuu Mtendaji**
**Kenyatta International Convention Centre**
**S.L.P 30746-00100**
**NAIROBI**

Au kuwekwa ndani ya sanduku la tenda lililoko kwenye Ghorofa ya Nne, KICC ili kufika mnamo au kabla ya **Februari 28, 2023 saa 4.30 asubuhi.**

**Stakabadhi za tenda zitafunguliwa papo hapo mbele ya waliotuma maombi au wawakilishi wao ambao wataamua kuhudhuria katika KICC Caucus 109. Wale waliotuma maombi mapema hakuna haja ya kutuma maombi upya.**

**Kaimu AFISA MKUU MTENDAJI**
**KENYATTA INTERNATIONAL CONVENTION CENTRE.**

Kenya Vision 2030

**“ Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa”**




# KWS yaanzisha mpango wa kuzuia zogo la binadamu na wanyama ziwani

**NA CHRIS MAHANDARA (KNA)**



**Catherine Wambani, naibu mkurugenzi wa KWS anayesimamia hifadhi ya magharibi. Picha|Chris Mahandara**

Shirika la Huduma za Wanyama Pori (KWS) limezindua mpango wa kuzuia ongezeko la visa vya mizozo ya wanyama na binadamu kwenye Ziwa Victoria.

Kupitia kampeni inayoitwa' Ufikiaji salama wa maji', KWS inapanga kuhamasisha watu wanaoishi ndani ya ukanda wa ziwa kunufaika kiuchumi na ziwa hilo bila kuzozana na wanyama pori

Naibu Mkurugenzi Mkuu wa KWS anayesimamia eneo la Magharibi Bi Catherine Wambani alisema kwamba mradi huo utakaotekelezwa pamoja na Serikali 13 za kaunti za eneo hilo utapunguza visa vya mizozo ya binadamu na wanyama.

Wambani alisema kwamba kupitia ushirikiano na serikali hizo, Mashirika ya Kijamii na umma, kampeni hiyo ya uhamasisho wa jinsi ya kuishi na wanyama itazidishwa katika eneo hilo. Hii, alisema, ni hatua ya muda mrefu ya kukabili athari hasi za tishio hilo na wakati huo huo kuokoa mamilioni ya pesa ambazo shirika hilo limekuwa likitumia kulipa fidia waathiriwa.

Kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita viwango vya maji katika Ziwa Victoria vimepanda na kusababisha kuongezeka kwa idadi ya mashambulizi ya wanyama pori.

Waathiriwa hasa wanaovamiwa na mamba, viboko na nyoka hufurika katika ofisi za KWS kutafuta fidia huku watu wa familia zinazopoteza wapendwa wao zikiachwa na majonzi.

“Maisha ya binadamu hayawezi kufidiwa. Hakuna kiasi cha pesa kinachoweza kufidia uhai wa mtu, majeraha na mateso,” alisema.

Wambani alisema hayo katika Chuo cha Mafunzo ya Leba cha Tom Mboya, Kisumu kwenye zoezi la kupata maoni ya umma kuhusu kubadilishwa kwa viwango vya ada za Mbuga za Kitaifa na hifadhi za wanyama.

Alisema kwamba mradi huo utakaoongozwa na Kamati za Kulinda Wanyama Pori za Kaunti zitakasimamiwa na makamishna wa kaunti, utatumiwa kama hatua ya kuzuia katika kuhakikisha kwamba wavuvi, watalii na watu wengine wanaotumia ziwa hilo kupata riziki wako salama.

KETRACO
Kenya Electricity Transmission Company Limited
*"Building a World Class National Grid"*

## NAFASI ZA KAZI

**UTANGULIZI**

Kampuni ya Kusambaza Umeme Kenya (KETRACO) ni shirika linalomilikiwa na serikali kwa 100%. lililoanzishwa tarehe 2 Desemba, 2008 chini ya Sheria ya Kampuni, Sura ya 486 kama Shirika la Serikali kwa mujibu wa Waraka wa Kipindi Na. 4 wa 2004 kuhusu Nishati. Majukumu ya Kampuni ni kupanga, kubuni, kujenga, kumiliki, kuendesha na kudumisha gridi ya usambazaji wa umeme wa msongo wa juu na viunganishi vya umeme vya kikanda.

Maono ya KETRACO ni kuwa kampuni ya kiwango cha kimataifa ya usambazaji umeme na kiunganishi kinachoongoza barani Afrika. Dhamira ya Kampuni ni kutoa usambazaji wa umeme wa kutegemewa, unaofaa na kukuza biashara ya kawi kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Kwa hili, Kampuni inakaribisha maombi kutoka kwa watu wanaofaa kujaza nafasi zifuatazo:

| No | Nafasi | Daraja | Idadi | Mfumo | Namba ya Marejeleo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Meneja Mkuu, Uendeshaji na Matengenezo ya Mfumo | KET 3 | 1 | Mkataba | KET/5/1C/40/15- B/VOL II |
| 2. | Meneja, Uhakikisho wa Ubora na Usimamizi wa Hatari | KET 4 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/157-B/Vol I |
| 3. | Meneja, Mikataba ya Huduma za Kisheria na Utawala | KET 4 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/148 -B/VOL I |
| 4. | Mchambuzi Biashara na Malipo ya HCM | KET 6 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/158-B/Vol I |
| 5. | Afisa Usalama -Uchunguzi | KET 6 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/145-B/Vol I |
| 6. | Afisa wa Bima | KET 6 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/144-B/Vol I |
| 7. | Afisa Sheria, Huduma za Uzingatiaji | KET 7 | 1 | P&P | KET/5/1C/40/156-B/VOL |
| 8. | Mhandisi Mhitimu wa Mafunzo-Umeme | KET 7 | 20 | P&P | KET/5/1C/40/63-B/Vol IV |
| 9. | Waendeshaji wa Kituo kidogo - Mafundi | KET 8 | 15 | P&P | KET/5/1C/40/93-B/Vol III |

Maelezo ya kina ya kazi, vipimo na mahitaji mengine yamewekwa kwenye tovuti yetu **www.ketraco.co.ke**.

**KUMBUKA:**

i. Uteuzi wa nafasi Na. 1 ni kwa masharti ya mkataba wa miaka mitano (5) na unaweza kurejeshwa kulingana na utendaji;
ii. Maombi yote kutoka kwa wagombea wanaovutiwa na waliohitimu lazima yawasilishwe kwa njia ya mtandao.
iii. Tutawasiliana na wagombea watakaoorodheshwa pekee.
iv. KETRACO haitozi ada yoyote kwa kutuma maombi, usindikaji, usaili au ada nyingine yoyote kuhusiana na mchakato wetu wa kuajiri.
v. KETRACO ni mwajiri anayetoa fursa sawa aliyejitolea kujumuisha jinsia na ulemavu. Watu wenye Ulemavu wanahimizwa kutuma maombi.

Waombaji walio na nia na waliotimiza masharti yanayohitajika wanapaswa kutuma maombi yao kwa uwazi yakionyesha nafasi iliyoombwa na Namba ya Kumbukumbu ya Nafasi. kupitia **kiungo cha kazi** kilichowekwa kwenye tovuti ya KETRACO na kuambatanisha nakala za vyeti na nakala, wasifu wa sasa na ushuhuda mwingine wowote unaofaa, mawasiliano ya simu, anwani ya barua pepe na wadhamini watatu (3) na maelezo ya mawasiliano yao ili kufikia anwani iliyo hapa chini kwa kufikia **Jumanne, tarehe 28 Februari 2023 saa 5:00PM EAT.**

REPUBLIC OF KENYA

## MINISTRY OF LABOUR AND SOCIAL PROTECTION

**STATE DEPARTMENT FOR LABOUR AND SKILLS DEVELOPMENT**

## TENDER NOTICE

The State Department for Labour and Skills Development invites sealed tenders from eligible bidders for the tenders detailed below:

| S/NO | REFERENCE NUMBER | REFERENCE NAME | ELIGIBILITY |
|---|---|---|---|
| 1. | ML&SP/SDL/ONT/002/2022-2023 | Provision of Security Services for the Ministry of Labour and Social Protection | Open to all eligible tenderers |
| 2. | ML&SP/SDL/ONT/003/2022-2023 | Provision of Cleaning Services for the Ministry of Labour and Social Protection | Preference groups Tender is reserved for preference groups under the Access to Government Procurement Opportunities (AGPO) scheme (Youth, Women and Persons with Disability) |

Qualified and interested eligible candidates may obtain further information and inspect the tender document at the **Supply Chain Management Office of the State Department for Labour and Skills Development** located at NSSF Building, Block A, Eastern Wing, 14th Floor during normal working hours.

A complete set of the tender document may be downloaded from the government tender portal **www.tenders.go.ke** and the State Department's website **www.labour.go.ke** ***for free.*** No tenders will be issued physically from the State Department.

Prices quoted should include all taxes, must be expressed in Kenya shillings and shall remain valid for a period of 120 days from the closing date of the tender.

All tenders for security services shall be accompanied by a tender security as detailed in the tender document and must be valid for a period of 150 days from the date of tender opening.

The tenderer shall chronologically serialize all pages of the tender document submitted including their attachments/testimonials.

Duly filled tender documents are to be tape bound and enclosed in a plain sealed envelope, marked with the tender number and name and be deposited in the tender box marked ***“Ministry of Labour and Social Protection”*** located at **NSSF Building, Block A, Eastern Wing, 14th floor** or be addressed and posted to:

**Principal Secretary**
**State Department for Labour and Skills Development**
**P.O. Box 40326-00100 NAIROBI**

So as to be received on or before **Tuesday 28th February 2023 at 1000hrs.**

Late tenders will be rejected.

Tenders will be opened immediately after the closing date and time in the presence of the tenderers and/or their representatives who may choose to attend the opening at the Boardroom located at **NSSF Building, Block A, Eastern Wing 7th floor.** Only one representative per tenderer shall be allowed to participate in the exercise in compliance with MOH protocols in combating COVID 19 Pandemic.

During the tender opening, tenderers will be required to submit one (1) original hard copy of the duly filled tender document clearly marked **“ORIGINAL”** and one (1) copy which should be a replica copy of the original clearly marked **“COPY”.**

There will be a mandatory a pre-arranged pre-tender site visit scheduled to be held from Monday 20th February, 2023 to 24th Friday 2023 as follows;

1. For Security services, this will be at the National Social Protection Secretariat (NSPS) offices ACK House, Bishop Road, opposite NSSF Building and at the Directorate of Occupational Safety and Health Services (DOSHS) offices at Safety House located in Industrial Area, along Commercial Street - Nairobi.

2. For Cleaning services, this will be at NSSF Building, Blocks AB&C, ACK House along Bishop Road, opposite NSSF Building, Directorate of Occupational Safety and Health Services (DOSHS) offices at Safety House, located in Industrial Area, along Commercial Street - Nairobi.

The Procuring Entity reserves the right to cancel the tender proceedings any time before notification of contract award.

**Head /Supply Chain Management Services**
**FOR: PRINCIPAL SECRETARY**

KENYA VISION 2030

MyGov.
FEBRUARI 14, 2023
NAIROBI-KENYA I TOLEO No. 31/2022-2023

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: info@information.go.ke

# Egerton yavumbua mimea inayohimili kiangazi na kuzalisha mavuno mengi

**NA JANE NGUGI (KNA)**



Chuo Kikuu cha Egerton kwa ushirikiano na wadau wa kibinafsi na umma kimevumbua aina ya mimea inayotoa mavuno mengi na inayostahimili ukame na maradhi huku kikiendeleza juhudi za kuwafunza wakulima wakumbatie mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Miongoni mwa aina zinazotoa mavuno mengi na kustahimili ukame zilizoruhusiwa sokoni na taasisi hiyo ni pamoja na Egerton Mbaazi M1, Mbaazi M2 Mbaazi 3 na Mbaazi M4), aina mpya 29 za mhongo , aina mpya za maharagwe za Tasha, Ciankui na Chelalang ambazo zinastahili kwa maeneo yenye joto na mbegu za njugu aina ya Nyota na Mwangaza.

Zingine ni aina mpya za mtama za EUS 130, EUS1, EUSS-10 na 'EU-SS-11 na mbaazi (Saina kal).

Mkurugenzi wa Bustani ya Kilimo -Sayansi wa Chuo Kikuu cha Egerton Profesa Paul Kimurto alisema kwamba kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, wadudu na maradhi ambayo hayakuwa au yaliyokuwa nadra yanaongezeka na kuathiri mavuno na kusababishia wakulima hasara. Profes Kimurto alisema kwamba kutokana na hali ya mabadiliko ya tabia nchi inayoshuhudiwa, Chuo Kikuu hicho na washirika wake, kimejitahidi kufanya utafiti na kupata aina zinazoweza kuzoea athari za hali ya anga. “Mabadiliko ya Tabia nchi yamekuwa tisho kwa utoshelevu wa chakula kote ulimwenguni. Athari zake zinajumuisha mvua isiyotabirika, na kupelekea mavuno kupungua na kuongezeka kwa gharama ya ya uzalishaji. Tukikosa kusaidia wakulima wetu kukumbatia kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabia nchi, uzalishaji utaendelea kupungua, na kusababisha mapato kupungua, watu kukosa kazi na njaa,” alieleza.

Kwa kufanya utafiti na kukuza mbegu zinazostahimili mabadiliko ya tabia nchi, Chuo Kikuu cha Egerton kimekuwa kikishirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mimea kwa Maeneo Kame ya Kitropiki (ICRISAT), Shirika la Kukagua Ubora wa Mimea (Kephis), Mradi wa Utafiti wa Jamii (CARP+) na Shirika la Utafiti wa Kilimo na Ufugaji Kenya (KALRO).

Mashirika mengine ni Kituo cha Usimamizi wa Ubora katika Kilimo na Kilimobiashara Endelevu (CESAAM), kampuni ya East African Breweries Limited (EABL), Shirika la Ukanda la Kujenga Uwezo wa Vituo Vikuu katika Kilimo (RUFORUM), na Wakfu wa MasterCard na Alliance for a Green Revolution in Africa (Agra).

“Kunapaswa kuwa na ubunifu endelevu katika aina za mbegu zinazo stahimili ukame, aina zinatunza mazingira na usimamizi bora wa baada ya mavuno ili kupunguza hasara. Pia tumekuwa tukiwezesha wakulima waweze kufanya maamuzi yanayofaa kama kupanda wakati unaofaa na mumea unaostahili,” alisema Profesa Kimurto. Kulingana na mhadhiri huyo, matumizi ya ubunifu na tekinolojia za kilimo kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ni kwa wakulima wa mashamba makubwa pekee.

## KWA UFUPI

### Wasichana wanaojifungua waanza kurejeshwa shuleni

MKE wa Gavana wa Kakamega, Prof Janet Kasili Barasa ametanza kampeni ya kuwatafuta wasichana matineja waliojifungua watoto na kuacha shule baada ya kupata mimba ili warudi shule kuendelea na elimu. Wasichana hao watakuwa wakiongoza kampeni dhidi ya mimba za matineja katika jamii na wale watakaotambuliwa watajiunga na shule za sekondari au wasaidiwe kujiunga na Vyuo vya Kifundi na mafunzo Anuai (TVET) wanazochagua ili waendeleze ndoto zao

Kupitia ziara zizopangwa katika nyumba zao wiki jana, Profesa Kasili alitambua wasichana 60 waliojifungua watoto kote katika kaunti hiyo, mmoja kutoka kila wadi kuwa waanzilishi wa mpango huo huku akihimiza washirika wengine kuunga wito wa kuchukua mama tineja kupitia kujitolea kusaidia mama tineja.

Washirika wengine waliohudhuria hafla ya kuzindua mpango huo walitaja idadi ya mama matineja watakaosaidia. Mashirika hayo yalikuwa Benki ya Kenya Commercial (KCB), Kampuni ya sukari ya Kabras, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro (MMUST), watu binafsi na wafanya biashara.

Prof Barasa hata hivyo alionya kwamba mpango huo haunuiwi kuhimiza wasichana matineja kupata mimba lakini kusaidia wale ambao tayari wanateseka kwa kupata mimba wakiwa na umri mdogo kutimiza ndoto zao.

Alisema kwamba mimba za mapema huwa zinaweza wasicbana wadogo kwenye hatari ya afya duni ya uzazi na watoto, kutengwa na jamii, utunguaji mimba usio salama, kukosa kuendelea na masomo, umasikini na hata kifo.

Kulingana na ripoti ya Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) ya mwaka wa 2022 idadi ya wasichana wa umri wa kati ya miaka 15-19 wanaojifungia imepungua kwa zaidi ya asilimia 30 kutoka 65 hadi 43 kwa kila wasichana matineja 1000. Kuwa kuendelesha kampeni kali dhidi ya mimba za matineja, Kakamega imepunguza mimba za wasichana matineja kwa walio na umri wa kati ya miaka 10-19 years kutoka 16 969 mwaka wa 2018 hadi 12 000 mwaka wa 2022 huku kaunti ndogo ya Malava ikiongoza kwa visa 1361 kulingana na data kutoka idara ya afya , Kakamega.

*NA Moses Wekesa (KNA)*

### IGAD kujadili mabadiliko ya tabia nchi huku ukame mrefu ukiathiri jamii vibaya

Mamlaka ya Ushirikiano wa Serikali kuhusu Maendeleo (IGAD) itaitisha mkutano wa kikanda wa hali ya anga baadaye mwezi huu huku athari za mabadiliko ya tabia nchi zikiendelea kuathiri mamilioni kote katika eneo hilo.

Mkutano huo, utakaofanyika Februari 20 2023, utajadili miongoni mwa mambo mengine, hali ya ukame unaoendelea ambao umezidisha uhaba wa chakula katika eneo la Upembe wa Afrika. Watu wapatao 36.1 milioni katika ukanda wa IGAD wameathiriwa na ukame wa sasa na wanakabiliwa na viwango vya juu vya uhaba wa chakula kulingana na takwimu.

Ukame huo pia unasemekana kuua mifugo takriban 4.2 milioni, kuharibu vyanzo ya riziki vya jamii za wafugaji na kuzilemaza kiuchumi kote katika ukanda huo. Hii imetajwa kama changamoto kuu kwa bara ikizingatiwa kwamba ukanda huu una karibu asilimia 50 ya mifugo Afrika chini ya jangwa la Sahara na mifugo huchangia takriban asilimia 15 ya pato la eneo hilo.Hivyo basi, IGAD imependekeza kutekeleza hatua kadhaa kushughulikia hali hii mbaya ikiwemo kuitisha kikao cha kikanda. “Mkutano huu utakuwa sehemu ya juhudi zetu tunazoendeleza eneo linalofahamu zaidi hali ya anga katika bara na kuinua uwezo wa mataifa wanachama kukusanya na kushughulikia data za kutabiri janga, ili kupunguza pengo kati ya onyo la mapema na hatua za mapema,” alisema Katibu Mkuu wa IGAD, Workneh Gebeyehu. “Tayari, tumepata ushahidi wa ufanisi wa mbinu hii. Katika miaka ya 2021 na 2022, tumeridhishwa na mpango wetu wa 'kupeleka data kwa watu' umeinua onyo kwa wakati ufaao,” alisema .

Alitaja 2020 na 2021 kama miaka migumu sana katika historia ya IGAD, akisema kwamba kipindi hicho ni chenye joto, kavu na chenye mizozo mingi katika siku za hivi majuzi.

Wakati huo huo, IGAD iliteua Wakenya watatu miongoni mwa watu 12 mashuhuri kuwa wanachama wa Baraza la Watu Mashuhuri la Mamlaka ya Ushirikiano wa Serikali kuhusu Maendeleo.

*Na Mohamed Hassan (KNA)*

# Mtandao mpya wa kusaidia biashara ndogo za kilimo kwa shughuli za kifedha wazinduliwa

**NA ANNE MWALE NA DENNIS RASTO(KNA)**

Kampuni kubwa ya kimataifa ya tekinolojia ya fedha, Avenews Fintech, imezindua apu ya simu za mkono kusaidia biashara ndogo katika kilimo (Agri-SMEs) kaunti ya Nakuru kuendesha shughuli za kifedha kama vile ulipaji dijitali, pochi ya mtandao na benki dijitali.

Afisa wa nyanjani wa kampuni hiyo Bw Timothy Kibet alisema kwamba wanashirikiana na taasisi kadha za kifedha za humu nchini kuwezesha biashara za kilimo katika maeneo ya mashambani kupata huduma pana za kifedha. Hizi ni pamoja ns kupata mikopo nafuu hata kama hawana huduma za benki za kawaida kupitia huduma zinazotolewa na Avenews. Alisema biashara ndogo za kilimo ndizo zinachangia ukuaji wa uchumi wa Kenya, huku mahitaji yao ya kifedha yakikosa kutimizwa.



**Baadhi ya wamiliki wa mashirika madogo ya kilimo biashara (Agri-SMEs) wakati wa uzinduzi wa apu ya simu ambayo itawezesha shughuli za kifedha kama ulipaji kidijitali.** PICHA: DENNIS RASTO

Bw Kibet alisema kwamba kupitia Avenews, biashara ndogo za kilimo zitaweza kufanya maamuzi ya kifedha kwa kutegemea habari na kupata mikopo itakayozisaidia kuafikia uwezo wao kikamilifu wa kibiashara.

Alihakikishia biashara ndogo Avenews imeundwa kuzirahisishia upatikanaji wa pesa zinazohitaji kununua pembejeo na mazao kwa njia ya kuendelea.

“Hii ni huduma ya kutgemewa, nafuu na ya haraka ya kufadhili biashara kilimo inayonuiwa biashara ndogo za kilimo. Matumizi yake bora yanaweza kuongeza mavuno, kupunguza gharama na kuimarisha maisha ya wakulima,” alisema Kibet.

Kulingana na Shirika la Kimataifa ya Kifedha (IFC), muda na gharama inayohitajika na dhamana ya mikopo nafuu kwa biashara na ugumu wa kuhudumia wakulima katika maeneo ya mashambani zinaweza kutatuliwa kupitia dijitali.

Kibet alisema ukosefu wa dhamana, gharama ya juu ya mikopo na muundo usio rasmi wa biashara umefanya biashara ndogo nyingi za kilimo kushindwa kupata mikopo, hali ambayo afisa huyo wa nyanjani alisema imezidishwa na janga la Covid-19.

REPUBLIC OF KENYA
GAA GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY
KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD
DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD
NHIF Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100
Tel: 0202715390 / 0757029456
Email: info@kenyayearbook.go.ke
www.kenyayearbook.co.ke